

KUWEKEZA KWENYE HUDUMA ZA UZAZI WA MPANGO KWA AJILI YA AFYA YA MAMA NA MTOTO

JE WAJUA KUWA KATI YA MWAKA 2004 MPAKA 2010:

1. Akina mama 24 kati ya mia hawakupata huduma za uzazi kwa sababu ya kukosa pesa za kulipia matibabu?
2. Akina mama 19 kati ya mia hawakupata huduma za uzazi kwa sababu ya umbali mrefu kufika kwenye kituo?
3. Akina mama 48 kati ya mia walijifungulia nyumbani badala ya hospitali hivyo kuhatarisha maisha yao na watoto?
4. Akina mama wajawazito 43 kati ya mia ndio wanaenda kupata huduma ya kliniki mara nne na zaidi kama ilivyopendekezwa na shirika la afya duniani?. Hii imepungua kutoka 63 kati ya mia mwaka 2004?
5. Zaidi ya nusu ya akina mama wajawazito (65 kati ya mia) hawakupimwa baada ya kujifungua; ni 31 kati ya mia tu walipimwa ndani ya siku mbili baada ya kujifungua. Wengi wa wale ambao hawakupimwa walikuwa ni masikini sana (76 katika kila mia) hali hii huonyesha kuwa masikini hawapati huduma?
6. Watoto 76 kati ya mia ya wale masikini zaidi walipatiwa chanjo zote ikilinganishwa na 84 kati ya mia ya wale wenye kipato kikubwa?
7. Vifo vya watoto hupungua jinsi muda kati ya mimba na mimba unavyoongezeka?, mfano vifo vya watoto chini ya miaka mitano hupungua kwa zaidi ya nusu kama mimba zikipishana kwa miezi 36.

PIA WAJUA KWAMBA:

Serikali imeazimia kwenye MKUKUTA II kuwa hadi kufikia mwaka 2015, akina mama 60 kati ya mia wanaohitaji huduma za uzazi wa mpango wawe wanazipata?. Lengo hili likifikiwa, litachangia:


- Ongezeko la upatikanaji wa huduma ya uzazi wa mpango kwa walio masikini ambapo uhitaji umeongezeka kutoka asilimia 24 hadi 30 kati ya mwaka 2005 na 2010.
- Kupunguza vifo vya uzazi toka vifo 454 (mwaka 2010) hadi angalau vifo 193 kwa kila vizazi 100,000 kufikia 2015. Hii ni kwa sababu imekadiriwa kwamba matumizi sahihi ya uzazi wa mpango yanaweza kuzuia mimba zisizotarajiwa milioni moja na nusu, kuzuia utoaji wa mimba hatari na kuzuia vifo vya uzazi karibu 5,116 ifikapo mwaka 2015.
- Kupungua kwa vifo vya watoto kutoka 112 hadi 45 katika kila vizazi 1,000 hadi mwaka 2015 kwa sababu imekadiriwa kuwa matumizi sahihi ya uzazi wa mpango yanaweza kuzuia karibu ya asilimia 30 ya watoto waliozaliwa na maambukizi ya VVU.
- Ongezeko la matumizi ya uzazi wa mpango linaweza kupunguza vifo vya uzazi kwa asilimia 20 hadi 35.

BAJETI ZA UZAZI WA MPANGO NA HUDUMA YA MAMA NA MTOTO

- Bajeti ya sekta ya afya ilikuwa kubwa mwaka 2007 (10.8%) na sasa ni imepungua mpaka 8.9%.
- Jumla ya bilioni 98.7 ilitengwa kwa ajili ya huduma ya Mama na Mtoto pamoja uzazi wa mpango kwa mwaka 2011/2012 ambapo ilipungua kutoka bilioni 229.2 iliyotengwa mwaka 2010/2011. Upungufu huu umetokea zaidi katika matumizi ya Malaria. Katika mwaka 2011/2012 matumizi ya serikali na ya wafadhili katika huduma ya mama na mtoto yamepungua. Huduma ya mama na mtoto imepata asilimia 19 ya bajeti yote ya mwaka 2010/2011 na kupungua hadi asilimia 8 mwaka 2011/2012.

¹Family Planning Outreach Programme Tanzania, 2011

- Katika bajeti nzima ya huduma ya mama na mtoto, mradi wa MMR² umepata asilimia 43 ya bajeti yote kwa mwaka 2011/2012, ingawa haina mchango wa moja kwa moja katika huduma ya mama na mtoto.
- Bajeti ya serikali kwa huduma ya mama na mtoto ilipungua kutoka bilioni 9.5 mwaka 2010/2011 mpaka bilioni 4.9 (upungufu wa zaidi ya asilimia 50) kwa mwaka 2011/2012 ikionyesha kuwa kitengo hicho hakijapewa kipaumbele.
- Serikali imeweka ongezeko la bajeti katika uzazi wa mpango kutoka bilioni 0.5 kwa mwaka 2010/2011 kufikia hadi bilioni 1.2 mwaka 2011/2012 wakati mahitaji sahihi ni bilioni 20 kwa mwaka. Hata hivyo mpaka mwisho wa Juni 15 2012 serikali haikuwa imetoa pesa yoyote kwenye eneo hili.
- Jumla ya fedha za uzazi wa mpango katika MTEF (bilioni 5.2) na mchango wa DFID kupitia USAID (milioni 4.6) ambao inaweka jumla ya billion 9.7 kwa mwaka wa fedha 2011/2012.



JE NINI KIFANYIKE?

1. Serikali itenge fungu maalumu la fedha (kutoka kwenye vyanzo vyake na wafadhili) kupelekwa katika huduma ya mama na mtoto.
2. Serikali, kupitia wizara ya afya kuweka kiwango cha fedha kilicho sahihi katika sekta ya afya hadi kufikia asilimia 15 kama ilivyosainiwa katika azimio la Abuja.
3. Uongozi wa wizara ya afya kuweka uwiano wa fedha katika mikakati ya huduma ya mama na mtoto kwenye bajeti ya afya hadi angalau kufikia asilimia 25.

²Si kila matumizi yalilenga afya ya Mama na mtoto kwa sababu kulikuwa na vyandarua kwa watu wote nk

³Mradi huu unafadhiliwa na ADB ukilenga mkoa wa Tabora, Mara na Mtwara kwa sababu ya vifo vingi vya Mama na mtoto. Taarifa zilizopatikana zinaonyesha kuwa pesa hizi zitatumika kukarabati vituo vya afya 30, zahanati 80 na hospitali za wilaya 8 pamoja na kusaidia vyuo vya utabibu.

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:
Health and Development Tanzania

P.O.Box 65147

Dar Es Salaam

Email: advocacy@hdt.or.tz

